Dhana ya kutathmini ustahimilivu na usalama wa eneo la hifadhi ya jadi

Mwongozo wa kutumia dhana hii

Dhana hii hukusaidia kutathmini ustahimilivu na usalama wa eneo la hifadhi ya jadi kwa kuangalia ‘afya’ ya ‘nguzo zake tano muhimu’:

1. **nguvu ya jamii ya wamiliki**
2. **muunganiko au mahusiano kati ya jamii na eneo husika**
3. **utendaji kazi wa taasisi ya utawala**
4. **hali ya uhifadhi wa eneo lenyewe**
5. **mapato ya kujikimu na ustawi wa jamii**

Dhana hii ya Ustahimilivu na Usalama itatumika katika mijadala ya mashinani, ikiwezekana kwa msaada wa Timu ya uwezeshaji na kwa kuzingatia vikundi vidogo vya jinsia, umri, uhusiano na eneo, n.k.

Kwa kila ‘nguzo’, Timu huchochea tafakari ya kikundi kwa kutoa maswali machache muhimu na kuweka mjadala kuwa makini. Baada ya dakika 10 hadi 20 za kubadilishana maoni, ushahidi na uzoefu, Timu itauliza 'swali muhimu' mtambuka kuhusu nguzo, ambalo litajibiwa kwa pamoja kulingana na kiwango cha ubora (k.m., kutoka 'haipo' hadi 'kuwa na nguvu sana au afya'). Ikiwa itatakiwa, kipimo cha ubora kinaweza kutafsiriwa katika alama ya herufi/tarakimu (k.m. kipimo cha 0 - 5), kama inavyoonyeshwa hapa chini.

0 - Haipo	1 - Ni dhaifu au imeharibiwa	2 – Dhaifu kiasi imeharibiwa	3 – Wastani au imechanganyika	4 – Imara kiasi au ina afya	5 - Imara sana na ina afya.

Alama siyo muhimu hata kidogo. Kilicho muhimu ni kuelewa jinsi kila 'nguzo' ilivyo na afya, na kwa nini. Ikiwa ni ‘dhaifu’, ni udhaifu gani mkubwa na unachangiwa na nini? Ikiwa ina ‘nguvu’, nguvu hizo ni zipi na huchangiwa na nini? Je, kuna matishio ya sasa au yanayotarajiwa au fursa zinazodhoofisha au kuimarisha masuala haya? Nakadhalika…

Timu inapaswa kuchukua maelezo yote ya kina kuhusu masuala yaliyoibuliwa wakati wa majadiliano, maoni mbalimbali yanayoweza kutolewa na mapendekezo yoyote yanayoweza kutolewa.

Mwishoni mwa kutumia dhana, 'alama ya jumla' inaweza kuwekwa kwa kujumlisha alama zote za nguzo tano, kama inavyoonyeshwa hapa chini. Alama ya muhtasari itakuwa kati ya 0 na 25, na itatoa kadirio la ustahimilivu na usalama wa eneo husika. Kiashirio hiki kitakuwa mahususi kwa jamii na kinaweza kutumika kuangaliwa baada ya mwaka mmoja au zaidi ili kuona kama mambo yameboreka/yanaonekana kuwa bora Zaidi au la. Alama haziwezi kulinganishwa katika maeneo tofauti, kwa kuwa zinategemea kikamilifu muktadha na mchakato wenyewe.

0 – 5 Siyo salama au stahimilivu	5 - 10 Haiko salama, ustahimilivu wa chini	10 – 15 Siyo salama kiasi, ustahimilivu wa chini	15-20 Salama kwa kiasi cha kutosha na stahimilivu	20-25 Usalama wa hali ya juu na stahimilivu

Nguzo ya 1: Uadilifu na nguvu ya jamii ya wamiliki

Maswali ya majadiliano

- Jamii yetu ina hisia ya utambulisho mmoja na tunu zinazokubalika na wote, kwa kuzingatia eneo husika?
- Kuna matukio maalum, sherehe, shughuli au taratibu zinazoonekana kuuweka hai na kuimarisha utambulisho wetu wa pamoja na mshikamano wa ndani?
- Hii inatofautiana kati ya vikundi katika jamii yetu—k.m., wanaume na wanawake, wazee na vijana, makabila madogo, aina ya maisha, mali au vikundi vya lugha?
- Jamii yetu inaweza kupanga maelewano ya ndani kuhusu masuala muhimu yanayoathiri maisha yetu na eneo letu?
- Jamii yetu inaona mienendo yoyote yenye kutia mashaka au chanya katika suala la uadilifu wetu kwa ujumla, hisia ya muunganiko wa pande zote, na wajibu kwa eneo letu?

Dodoso za mjadala (Masuala gani muhimu yaliibuliwa?

Swali muhimu la 1: Ni kwa kiasi gani watu katika jamii yako wanajisikia kuunganika na kuwajibika kila mtu kwa mwingine?		Jibu la kikundi: (maelezo)		**Muhtasari wa alama (0-5 kulingana na kipimo hapo chini)**	
0 Hakuna kabisa	1 Kidogo tu	2 Kwa kiasi fulani lakini inapungua	3 Wastani lakini kwa kutegemewa	4 Kwa wingi kabisa na inaongezeka	5 Kwa kiasi kikubwa

Nguzo ya 2: Muunganiko/mahusiano kati ya jamii na eneo lake

Maswali ya majadiliano

- Jamii yetu ina uhusiano wa muda mrefu na/au imara sana na eneo letu (au, angalau, na sehemu yake)?
- Wanajamii wanafahamu kuhusu eneo letu na vipengele vyake, na miunganiko muhimu inayotuunganisha nayo?
- Janajamii wetu wanafikiri eneo hilo ni muhimu? Je, kama jamii, iko tayari kulilinda na kulitetea, ikihitajika?
- Jamii yetu inaona mienendo yoyote ya wasiwasi au chanya katika suala la muunganiko wetu wa jumla na hisia ya kuwajibika kwa eneo letu?
- Hisia hii ya muunganiko inatofautiana kati ya vikundi katika jamii yetu—k.m., wanaume na wanawake, wazee na vijana, makabila madogo, aina ya riziki, itikadi, utajiri au lugha?
- Maarifa, ujuzi na mahusiano yanayohusiana na eneo husika yamerithishwa kutoka kwa wazee wetu hadi kwa vizazi vichanga? Je, hizo zimefanywa kwa undani na kuboreshwa kulingana na wakati?

Vidokezo vya mjadala (Masuala gani ya muhimu yaliibuliwa?)

Swali muhimu la 2: Je! dhamana ya jamii yetu au hisia ya uhusiano na eneo letu la jadi ni kubwa kiasi gani?		Jibu la kikundi (maelezo)			**Muhtasari wa alama (0-5 kulingana na kipimo hapo chini)**
0 Hakuna	1 Dhaifu kabisa	2 Ipo lakini inadhoofu	3 Ipo na iko imara	4 Ina nguvu na inaongezeka	5 Ina nguvu sana

Nguzo ya 3: Utendaji wa taasisi ya utawala
Maswali ya mjadala ▪ Kuna jtaasisi ya kufanya maamuzi kuhusu eneo letu husika(k.m. kanuni za kufikia na kutumia)? ▪ Taasisi zinazofanya maamuzi ni halali mbele ya macho ya jamii? Je, wanajamii wetu wako katika mshikamano na taasisi ya utawala ya eneo husika? Je, wanaheshimu maamuzi yake na kuyatetea, ikibidi? ▪ Taasisi ya utawala ya eneo lehusika inaweza kulinda utekelezaji wa maamuzi na kanuni zake yenyewe? ▪ Kuhusiana na swali lililotangulia, je, eneo lehusika lina mipaka? Je, eneo limepangwa/lina ramani? Je, linatambulika rasmi katika sheria za nchi au inaonekana katika hati zozote za kisera au ripoti za kitaifa? ▪ Je, jamii yetu inaona mienendo yoyote ya kutia mashaka au chanya katika suala la heshima ya jumla kwa jamii kujihusisha na utawala wa eneo hilo? ▪ Uhusika huo unatofautiana katika makundi ndani ya jamii yetu—k.m., wanaume na wanawake, wazee na vijana, makabila madogo, aina ya kipato/riziki zinazopatikana, mali au vikundi vya lugha? ▪ Vidokezo vya mjadala (Masuala gani muhimu yaliibuliwa?)

<u>Swali muhimu la 3:</u> Je, taasisi ya utawala ya eneo husika nafanya kazi vizuri kiasi gani?	Jibu la kikundi (maelezo)	**Alama (0-5 kulingana na kipimo hapo chini)**

0 Haifanyi kazi	1 Ni dhaifu	2 Inafanyakazi lakini inazorota	3 Inafanyakazi vizuri kwa wastani na ni imara	4 Inafanyakazi vizuri na inazidi kuwa imara zaidi	5 Ni taasisi yenye nguvu sana

Nguzo ya 4: Afya ya ikolojia na ubora wa eneo hilo

Maswali ya mjadala

- Ardhi, hewa, maji na maliasili zenye thamani ‘zina afya’ kiasi gani kwa jamii (k.m., ubora wa hewa na udongo; ubora na wingi wa maji safi; wingi na afya ya viumbe hai; wanyamapori, uvuvi, n.k.)?
- Je, mifumo ikolojia ina afya kwa kiasi gani (k.m. misitu, nyanda za malisho, maeneo yenye maji ya maeneo oevu, maeneo ya pwani, n.k.) ndani ya eneo letu la jadi au karibu nayo?
- Je, jamii yetu inaona mienendo yoyote inayotia mashaka au chanya katika suala la uadilifu wa ikolojia kwa ujumla na afya ya mfumo ikolojia wa eneo la hifadhi ya jadi?
- Je, hali na mweneno wa spishi muhimu zinazopatikana kipekee (mimea na wanyama) zikoje katika eneo letu la jadi? Je, kuna spishi zozote muhimu zinzopatikana kipekee zinazoonekana kustawi au kupungua kwa kiasi kikubwa?
- Je, zipo mandhari na/au mandhari ya bahari katika eneo letu la jadi zinazovutia? Kama zipo, je, zinabeba thamani na tabia na maadili yao ya kitamaduni, kijamii, kiroho au kidini kwa watu na jamii zetu?
- **Vidokezo vya mjadala** (Masuala gani muhimu yaliibuliwa?)

<u>Swali muhimu la 4:</u> Mazingira katika eneo husika yana afya kiasi gani?	Jibu la kikundi (maelezo)	**Alama (0-5 kulingana na kipimo hapo chini)**

0 Yameharibiwa vibaya	1 Yameharibiwa	2 Bado yapo vizuri lakini mwenendo siyo mzuri	3 Yapo vizuri na imara	4 katika hali nzuri na yanaimarika	5 Yanastawi

Nguzo ya 5: Mapato ya kujikimu na ustawi wa jamii

Maswali ya majadiliano

- Thamani ya mali zinazohusiana na eneo letu husika ziko salama kwa kiasi gani, kama vile chakula, maji, nyumba na rasilimali zinazotumika kujipatia vipato vya kujikimu au kupata mapato?
- Kuna ushahidi wowote unaoonyesha kuongezeka au kupungua kwa umaskini na ukosefu wa usawa katika jamii yetu? Je, kuna uhusiano wowote kati ya mienendo hii na eneo letu la hifadhi yetu?
- Afya ya jamii yetu kwa ujumla iko vipi? Je, kuna uhusiano wowote kati ya afya ya jamii yetu na uwepo na utunzaji wa eneo husika?
- Je! ni salama kiasi gani tunu zisizo za mali zinazohusiana na eneo letu la jadi, kama vile maadili ya kidini na kitamaduni, hali ya kuridhika na afya njema?
- Je, tunakabiliwa na mabadiliko ya kitamaduni, kuibuka kwa migogoro mipya, uhalifu, kutoheshimu maadili ya kimila, matukio makubwa ya uhamiaji, uharibifu au tabia ya kuiharibu? Je, mienendo hii kwa namna yoyote inahusiana na hali ya eneo hilo?
- Je, hii inatofautiana kati ya vikundi katika jamii yetu—k.m., wanaume na wanawake, wazee na vijana, makabila madogo, aina ya maisha, mali au vikundi vya lugha?

Vidokezo vya mjadala (Masuala gani muhimu yaliibuliwa?)

Swali muhimu la 5: **Je, ni kiwango gani cha ustawi wa jumla katika jamii yetu, hasa kwa wale ambao maisha yao yanategemea/yanaunganishwa moja kwa moja na eneo husika?**	Jibu la kikundi (maelezo)	**Muhtasari wa alama (0-5 kulingana na kipimo hapo chini)**

0 Ni mbaya kabisa	1 Ni mbaya	2 I Ni sawa lakini mwenendo wake siyo mzuri	3 Iko sawa na imara	4 Iko katika hali nzuri na inaendelea kuimarika	5 Inastawi